

## URAFIKI WA MASHAKA

Hapo zamani za kale palikuwepo marafiki wawili walioitwa Chonde na mwingine Choche.

Siku moja Chonde alikwenda nyumbani kwa Choche na kupora vitu vyote vya thamani alivyovihitaji kwa ubabe, kiburi, na dharau bila kujali kuwa ni rafiki yake. Ingawa Choche alijitahidi kujitetea huku akikumbusha urafiki wao uliokaribia undugu wa damu, Chonde hakukubali kumwachia vitu vya thamani. Alivichukua na kuondoka navyo kusikojulikana kisha kumwachia vitu vichache kwa masharti. Choche alikubali masharti hayo kwa unyonge, ilimradi rafiki yake aondoke amani irudi.

Kwa kuwa Chonde tayari alishachukua vitu vingi na vingine kuviharibu, Choche alibaki maskini na dhaifu kutokana na sonona.

Baada ya miaka mingi kupita, Chonde alidhuru nyumbani kwa rafiki yake ili kumjulia hali. Alimmkuta yu hoi kitandani, mgonjwa *wa leo wa kesho*. Ndipo Chonde alipomwambia Choche wafufue urafiki wao kisha kukubaliana

kumkopesha kiasi chochote cha fedha akitakacho lakini marejesho yatakuwa kwa riba. Na endapo umauti utamfika, atalea watoto wa Choche kwa kuwapa misaada mbalimbali ya kibinadamu ingawa masharti yataendelea. Ili aweze kurudisha hali yake ya kiuchumi, Choche alikubali.

Choche alipatwa na umauti na kwa sasa watoto wake wapo kwenye himaya ya Chonde wakiendelea kunolewa kifikra na kukumbushwa masharti na mikataba iliyosainiwa na Mzee Choche.

Ingawa kimwili watoto hao bado wanaishi karibu na kaburi la baba yao lakini fikra zao na matumaini yao juu ya maendeleo yanategemea mwongozo wa Bwana Chonde, rafiki wa Baba yao.